TANGAZO LA SERIKALI NA. 381 la tarehe 17/05/2024

SHERIA YA USAFIRISHAJI MAJINI
(SURA YA 165)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 284)*

KANUNI ZA UBEBAJI WA SHEHENA YA MIZIGO YABISI NA FUELI ZA MWAKA 2024

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
MASHARTI YA JUMLA KWA UBEBAJI WA SHEHENA YA MIZIGO YABISI

4. Ubebaji wa shehena ya mizigo yabisi tofauti na nafaka.
5. Taarifa za mizigo.
6. Uchunguzi wa oksijeni na kifaa cha kutambua gesi.
7. Matumizi ya dawa za kuua wadudu kwenye meli.
8. Uhifadhi na utunzaji.
9. Nyaraka ya masuala ya msingi ya usalama.
10. Katazo la kuchanganya shehena ya mizigo oevu na mchakato wa uzalishaji wakati wa safari baharini.

SEHEMU YA TATU
MASHARTI MAALUMU YA UBEBAJI KWA SHEHENA YA MIZIGO YABISI

11. Kukubalika kwa usafirishaji.
12. Upakiaji, upakuaji na uhifadhi wa shehena za mizigo.

SEHEMU YA NNE
UBEBAJI WA NAFAKA

13. Masharti ya meli ya mizigo inayobeba nafaka.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA JUMLA

14. Adhabu za jumla.
15. Tathmini na ripoti.
16. Ushughulikiaji wa malalamiko.

---

**MAJEDWALI**

---

SHERIA YA USAFIRISHAJI MAJINI
(SURA YA 165)

## KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 284)*

KANUNI ZA UBEBAJI WA SHEHENA YA MIZIGO YABISI NA FUELI ZA MWAKA 2024

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Ubebaji wa Shehena ya Mizigo Yabisi na Fueli za Mwaka 2024.

Matumizi

**2**.-(1) Kanuni hizi zitatumika kwa ubebaji wa mizigo ulioainishwa katika Sura ya VI ya Mkataba wa Usalama Baharini ambao, kutokana na hatari zake mahususi kwa meli au watu waliomo melini, unaweza kuhitaji tahadhari maalumu katika meli na katika meli ya mizigo ya chini ya tani 500 za uzito wa jumla:

Isipokuwa kwamba, Kanuni hizi zinaweza kutotumika katika meli za mizigo ya chini ya tani 500 za uzito wa jumla, endapo Shirika litaona kwamba asili na hali ya uhifadhi wa mizigo wakati wa safari zinaweza kusababisha matumizi ya masharti mahususi ya Kanuni hizi kutokuwa na ulazima au kutohitahitajika.

(2) Bila kuathiri ujumla wa kanuni ndogo ya (1), Kanuni hizi hazitatumika kwa-

(a) chombo cha starehe;

(b) meli ambayo haina nahodha, wafanyakazi au mlinzi;

(c) meli ya kivita au ya kijeshi;

(d) chomb kinachomilikiwa au kuendeshwa na Serikali kwa huduma zisizo za kibiashara;
(e) chombo cha uvuvi;
(f) vyombo vinavyobeba mizigo ya kimiminika na gesi kwa wingi; na
(g) vyombo vinavyobeba mizigo mingine ambayo imeainishwa katika Sura nyingine za Mkataba wa Usalama Baharini.

Tafsiri

**3**. Katika Kanuni hizi isipokuwa muktadha utahitaji vinginevyo-

"chombo cha kubebea mizigo" maana yake ni gari, kasha, flati, mbao za kubebea mizigo, tangi linalohamishika, chombo cha kufungia, au vifaa vingine vya kubeba mizigo au sehemu ya vifaa hivyo ambavyo vipo kwenye meli, na havijafungwa katika meli hiyo, na inajumuisha mzigo wenye magurudumu na chombo chochote cha kusafirishia mizigo;

"IMO" maana yake ni kama ilivyoainishwa katika Sheria;

"Kanuni za Kimataifa za Nafaka" maana yake ni Kanuni za Kimataifa za Usafirishaji Salama wa Nafaka kwa Wingi iliyopitishwa na IMO kwa azimio la namba MSC.23(59) kama linavyoweza kurekebishwa;

"Kanuni za IMSBC" maana yake ni Kanuni za Kimataifa za Baharini za Mizigo Yabisi inayobebwa kwa Wingi iliyopitishwa na IMO kwa azimio la MSC.268 (85), kama linavyoweza kurekebishwa;

"kasha" maana yake ni chombo cha kusafirishia-
(a) kinachotumika kwa matumizi ya kudumu na ambacho ni imara kuweza kutumika mara kwa mara;
(b) kilichotengenezwa maalum ili kuwezesha usafirishaji wa bidhaa, kwa njia moja au zaidi za usafiri, bila kupakiwa upya njiani;

(c) kilichotengenezwa kwa ajili ya kufungwa au kwa urahisi wa kubebwa, chenye vifaa kwenye kona zake kwa ajili hiyo;

(d) chenye ukubwa kiasi kwamba eneo lililopo katika kona nne za chini-

(i) liwe na angalau mita za mraba 14; au

(ii) liwe na angalau mita za mraba 7 ikiwa imefungwa viunga vya kona yake vya juu;

Isipokuwa, linapobebwa pamoja na chesisi, neno kasha halijumuishi gari au vifungashio;

"mafuta" maana yake ni kama ilivyoainishwa katika Sheria;

"fueli" maana yake ni mafuta yoyote yanayotumika kama nishati kuhusiana na kuendesha mitambo na mitambo saidizi ya meli ambamo mafuta hayo hubebwa;

"MARPOL" maana yake ni Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uchafuzi Mazingira kutoka Melini ya mwaka1973 na Itifaki zake za mwaka 1978 pamoja na marekebisho yake;

"meli ya mizigo" maana yake ni meli ambayo si meli ya abiria;

"Mkataba wa Usalama" maana yake ni kama ilivyoainishwa katika Sheria;

Sura ya 415 "Msajili" maana yake ni Msajili aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 31 cha Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania;

"nafaka" maana yake ni kama ilivyoainishwa katika Sheria;

"nafasi ya kuhifadhi mizigo" maana yake ni nafasi yoyote tangi au nafasi katika meli iliyotengwa kwa ajili ya kubeba mizigo;

"Notisi ya Usafirishaji Majini" maana yake ni Notisi ya Usafirishaji Majini iliyotolewa na Msajili na

inajumuisha rejea ya nyaraka yoyote inayorekebisha au kubadili Notisi hiyo;

"safari fupi ya kimataifa" maana yake ni kama ilivyoainishwa katika Sheria;

"shehena ya mzigo" maana yake ni mzigo uliobebwa kwa wingi;

"shehena ya mzigo yabisi" maana yake ni mzigo wowote tofauti na mzigo oevu au gesi, inayojumuisha mchanganyiko wa chembe ndogo, chembe kubwa au vipande vikubwa vya bidhaa kiujumla muundo wake unafanana, ambayo hupakiwa moja kwa moja kwenye nafasi za kuhifadhia mizigo za meli bila kuzuiwa na kizuizi chochote;

Sura ya 165

"Sheria" Maana yake ni Sheria ya Usafirishaji Majini;

Sura ya 415

"Shirika" maana yake ni Shirika la Wakala wa Meli lililoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania; na

"taarifa za mizigo" maana yake ni taarifa zinazohusiana na mzigo au uhifadhi wake ambao unaainisha tahadhari muhimu kwa ajili ya ubebaji wa mizigo kwa njia ya bahari.

## SEHEMU YA PILI
## MASHARTI YA JUMLA KWA UBEBAJI WA SHEHENA YA MZIGO YABISI

Ubebaji wa shehena ya mizigo yabisi tofauti na nafaka

**4**. Ubebaji wa shehena ya mizigo yabisi tofauti na nafaka utazingatia masharti husika ya Kanuni za IMSBC.

Taarifa ya mzigo

**5**.-(1) Msafirishaji atawasilisha kwa nahodha au mwakilishi wake taarifa sahihi kuhusu mizigo kabla ya kupakiwa ili kuwezesha tahadhari ambazo zinaweza kuwa muhimu kwa uhifadhi sahihi na ubebaji salama wa mizigo kuanza kutumika.

(2) Taarifa iliyorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) -

(a) itakuwa katika Fomu iliyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza; na

(b) itathibitishwa kwa maandishi na kwa nyaraka sahihi za usafirishaji kabla ya kupakia mzigo melini.

(3) Taarifa za mzigo zitajumuisha-

(a) ikiwa ni ya mzigo wa jumla na mzigo uliobebwa kwenye chombo cha kubeba mzigo-

(i) maelezo ya jumla ya mzigo;

(ii) uzito wa jumla wa mzigo au vyombo vya kubebea mzigo; na

(iii)sifa zozote husika za kipekee za mzigo;

(b) ikiwa ni ya shehena ya mzigo yabisi, taarifa kama zinavyohitajika na kifungu cha 4 cha Kanuni za IMSBC kuhusu tathmini ya kukubalika kwa mizigo kwa usafirishaji salama ikijumuisha-

(i) utambulisho na uainishaji;

(ii) utoaji wa taarifa;

(iii)cheti cha upimaji;

(iv)taratibu za sampuli; na

(v) muda kati ya uchukuaji wa sampuli na upimaji, upakiaji wa kikomo cha unyevu unaosafirishwa na utambuzi wa kiwango cha unyevu.

(4) Kwa madhumuni ya kanuni hii, taarifa ya mzigo inayotakiwa chini ya Sura ndogo ya 1.9 ya Kanuni za Taratibu za Uhifadhi na Utunzaji wa Mizigo, zitatolewa.

(5) Kabla ya upakiaji wa vyombo vya kubebea mizigo melini, msafirishaji atahakikisha kwamba uzito wa jumla ni kama ulivyoainishwa kwenye nyaraka za usafirishaji.

(6) Endapo mzigo umebebwa kwenye kasha,

isipokuwa kwa makasha yaliyobebwa kwenye chesisi au tela pale ambapo makasha hayo yanavutwa au kwenda au kutoka meli ya ro-ro inayojihusisha na safari fupi za kimataifa, uzito wa jumla kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo ya (3)(a) utahakikiwa na msafirishaji, kwa-

(a) upimaji wa uzito wa kasha lenye mzigo kwa kutumia kifaa kilichothibitishwa na kupitishwa; au

(b) upimaji wa uzito wa vifurushi na mizigo yote, ikijumuisha mbao za kubeba na kukalishia mzigo na vifaa vingine vya kuhifadhia vitakavyopakiwa kwenye kasha na kuongeza uzito wa kasha tupu kwa jumla ya uzito pekee, kwa kutumia njia iliyothibitishwa na iliyoainishwa chini ya Kanuni za Uzito wa Jumla Uliohakikiwa wa Kasha la Kubeba Mzigo.

TS.Na. 197 la 2016

(7) Msafirishaji wa kasha atahakikisha uzito wa jumla uliothibitishwa unatajwa kwenye nyaraka za usafirishaji zilizoainishwa chini ya Kanuni za Uzito wa Jumla Uliohakikiwa wa Kasha la Kubeba Mzigo.

TS.Na. 197 la 2016

(8) Nyaraka za usafirishaji-

(a) zitasainiwa na mtu aliyeidhiniwa na msafirishaji; na

(b) zitawasilishwa kwa naodha au mwakilishi wake na mwakilishi wa kituo cha bandari, kwa wakati na nahodha au mwakilishi wake, kutumika kwenye maandalizi ya mpango wa uhifadhi mizigo melini.

(9) Endapo nyaraka za usafirishaji, zinazohusu kasha lenye mzigo hazioneshi uzito wa jumla uliohakikiwa na naodha au mwakilishi wake na mwakilishi wa kituo cha bandari hawajapata uzito wa jumla uliohakikiwa wa kasha lenye mzigo, kasha hilo halitapakiwa kwenye meli.

(10) Nahodha anayepakia mzigo kwenye meli

bila taarifa sahihi zinazotakiwa chini ya kanuni hii anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua kiasi cha shilingi za Tanzania sawa na Dola za Marekani elfu mbili au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote.

Uchunguzi wa oksijeni na kifaa cha kutambua gesi

**6**. Naodha atahakikisha kwamba-

(a) kifaa sahihi cha kupima mgandamizo wa gesi au oksijeni kwenye hewa kinatolewa pamoja na maelezo ya kina ya utumiaji wake wakati wa kusafirisha shehena ya mzigo yabisi inayoweza kutoa sumu au gesi inayowaka au inayosababisha upotevu wa oksijeni katika eneo la kuhifadhi mizigo kwenye meli; na

(b) baharia anapata mafunzo ya matumizi ya kifaa hicho.

Matumizi ya dawa za kuua wadudu kwenye meli

**7**. Nahodha atahakikisha kwamba tahadhari sahihi zinachukuliwa kwenye matumizi ya dawa za kuua wadudu kwenye meli, hasa kwa madhumuni ya kuua wadudu.

Uhifadhi na utunzaji

**8**.-(1) Nahodha atahakikisha kwamba wakati wote wa safari, mzigo, vyombo vya kubebea mizigo na vyombo vya kusafirishia mizigo vilivyobebwa kwenye eneo la juu au chini ya deki vinapakiwa, kuhifadhiwa na kutunzwa ili kuzuia-

(a) uharibifu au hatari kwa meli na watu waliomo melini; na

(b) upotevu wa mizigo iliyopo melini.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mzigo, vyombo vya kubebea mizigo na vyombo vya kusafirishia mizigo vitafungwa na kuhifadhiwa ndani ya chombo, ili kuzuia, wakati wote wa safari uharibifu au hatari kwa meli na watu waliopo melini.

(3) Nahodha wa meli atachukua tahadhari stahiki

wakati wa upakiaji na usafirishaji wa mizigo mizito au mizigo yenye vipimo visivyo vya kawaida ili kuhakikisha kwamba-

(a) hakuna uharibifu wa muundo wa meli unaotokea; na

(b) uelea thabiti wa meli wa kutosha unadumishwa wakati wote wa safari.

(4) Nahodha atachukua tahadhari stahiki wakati wa upakiaji na usafirishaji wa vyombo vya kubebea mizigo na vyombo vya kusafirishia mizigo kwenye meli za ro-ro, kuhusiana na-

(a) kuweka mipangilio kwenye meli hiyo na vyombo vya kubebea mizigo na vyombo vya kusafirishia mzigo; na

(b) uimara wa maeneo yaliyotengwa na mpangilio wa mizigo.

(5) Nahodha atahakikisha kwamba makasha ya mizigo hayapakiwi kupita zaidi ya uzito wa jumla wa juu uliyoainishwa kwenye kibao cha idhini ya usalama kama ilivyoainishwa chini ya Kanuni za Uzito wa Jumla Uliohakikiwa wa Kasha la Kubeba Mzigo.

TS. Na 197 la 2016

(6) Nahodha atahakikisha kwamba mizigo yote tofauti na shehena ya mizigo yabisi na oevu, vyombo vya kubebea mizigo na vyombo vya kusafirishia mizigo, inapakiwa, kuhifadhiwa na kutunzwa wakati wote wa safari kwa mujibu wa Mwongozo wa Utunzaji Mizigo.

(7) Nahodha atahakikisha kwamba katika meli yenye nafasi za ro-ro, utunzanji wa mizigo inayorejewa chini ya kanuni ndogo ya (6), itajazwa kabla ya meli kuondoka kutoka kwenye gati kwa mujibu wa Mwongozo wa Utunzaji Mizigo.

(8) Shirika litahakikisha kwamba Mwongozo wa Utunzaji Mizigo umeandaliwa kwa kiwango sawa na Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

(9) Nahodha anayeshindwa kupakia, kuhifadhi na kutunza mzigo, vyombo vya kubebea mzigo na vyombo

vya kusafirishia mzigo kama inavyohitajika chini ya kanuni hii anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi za Tanzania sawa na Dola za Marekani elfu mbili au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote.

Nyaraka ya masuala ya msingi ya usalama

**9**. Nahodha atahakikisha kwamba meli inayobeba mafuta au fueli, inapatiwa nyaraka ya masuala ya msingi ya usalama, kwa kuzingatia mapendekezo ya IMO kuhusu Nyaraka ya Masula ya Msingi ya Usalama kwa mizigo na mafuta ya kuendeshea mitambo ya meli katika Kiambatisho cha I cha MARPOL, kabla ya kupakia mafuta hayo kama shehena ya mzigo au ujazaji wa fueli melini.

Katazo la kuchanganya shehena ya mizigo oevu na mchakato wa uzalishaji wakati wa safari baharini

**10**.-(1) Nahodha atahakikisha kwamba hakuna uchanganyaji wa shehena ya mizigo oevu wakati wa safari baharini.

(2) Katazo linalorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1), halitatumika kwa-

(a) mchanganyiko wa bidhaa kwa matumizi katika utafutaji; na
(b) utumiaji wa rasilimali za madini yaliyopo chini ya bahari kwa ajili ya kuwezesha shughuli hizo.

(3) Nahodha atahakikisha kwamba hakuna mchakato wa uzalishaji melini wakati wa safari za baharini.

(4) Katazo linalorejewa chini ya kanuni ndogo ya (3) halitatumika kwa-

(a) mchakato ya uzalishaji wa mizigo kwa matumizi katika utafutaji; na
(b) utumiaji wa rasilimali za madini yaliyopo chini ya bahari kwa ajili ya kuwezesha shughuli hizo.

(5) Kwa madhumuni ya kanuni hii-

(a) ”uchanganyaji wa kifizikia” maana yake ni

mchakato ambao pampu za mizigo za meli na bomba vinatumika kusambaza mizigo miwili au zaidi tofauti ndani ya meli kwa lengo la kupata bidhaa mpya; na

(b) ”mchakato wa uzalishaji” maana yake ni uendeshaji wa kukusudia ambao unapelekea mabadiliko ya kikemikali kati ya mzigo wa meli na dutu nyingine kutokea.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI MAALUMU YA UBEBAJI WA SHEHENA YA MIZIGO YABISI

Kukubalika kwa usafirishaji

**11**. Nahodha atahakikisha kabla ya kupakia shehena ya mzigo yabisi, ana taarifa inayojitosheleza kuhusu uelea thabiti wa meli na mgawanyo wa mizigo kwa kuzingatia masharti ya viwango vya upakiaji.

Upakiaji, upakuaji na uhifadhi wa shehena za mizigo

**12**.-(1) Nahodha atahakikisha kwamba meli inapewa kitabu ambacho kimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza, kwa madhumuni ya kumwezesha kuzuia mkandamizo kwenye umbo la meli.

(2) Kitabu kilichorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1), kitajumuisha-

(a) data ya uelea thabiti, kama inavyohitajika chini ya kanuni ya II-1/5-1 ya Mkataba wa Usalama;

(b) kiwango na uwezo wa kujaza na kutoa maji katika farumi;

(c) kiwango cha juu cha mzigo kinachoruhusiwa kwa kila kizio cha eneo la uso wa pleti ya juu ya tangi;

(d) kiwango cha juu cha mzigo kinachoruhusiwa kwa eneo la kuhifadhia mzigo;

(e) maelekezo ya jumla ya upakiaji na upakuaji kuhusiana na uimara wa umbo la meli

ikijumuisha vizuizi vyovyote vya hali mbaya zaidi za uendeshaji wakati wa upakiaji, upakuaji, shughuli za farumi na safari;

(f) katazo lolote maalumu kama vile ukomo uliowekwa na Msajili kupitia Notisi ya Usafiri Majini; na

(g) ambapo mahesabu ya uimara yanahitajika, kiwango cha juu cha nguvu na uelekeo wake unaoruhusiwa kwenye umbo la meli wakati wa upakiaji, upakuaji na safari.

(3) Kabla ya shehena ya mzigo yabisi haijapakiwa au haijapakuliwa, nahodha na mwakilishi wa kituo cha bandari watakubaliana juu ya mpango wa kupakia na kupakua ili kuhakikisha kwamba nguvu na uelekeo unaoruhusiwa wa meli haujazidishwa wakati wa kupakia au kupakua, ikijumuisha-

(a) mfuatano;

(b) kiasi na kiwango cha kupakia au kupakua, kwa kuzingatia kasi ya kupakia au kupakua; na

(c) kiasi cha uwekaji na umwagaji maji katika farumi ya meli.

(4) Mpango uliorejewa chini ya kanuni ndogo ya (3), na marekebisho yoyote yatakayofuata yatawasilishwa kwa Mamlaka ya Bandari.

(5) Nahodha wa meli na mwakilishi wa kituo cha bandari atahakikisha kwamba shughuli za upakiaji na upakuaji zinafanywa kwa mujibu wa mpango uliokubaliwa.

(6) Endapo wakati wa kupakia au kupakua ukomo wowote uliorejewa chini ya kanuni ndogo ya (2) unazidi au kuna uwezekano wa kuzidi ikiwa kupakia au kupakua kunaendelea, nahodha atasitisha shughuli na kuitaarifu Mamlaka ya Bandari.

(7) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (6) nahodha na mwakilishi wa kituo cha bandari watahakikisha

kwamba-

(a) hatua za kurekebisha zinachukuliwa wakati wa kupakua mzigo; na

(b) njia za upakuaji haiharibu umbo la meli.

(8) Nahodha atahakikisha kwamba-

(a) mabaharia wanaendelea kufuatilia shughuli za kupakia na kupakua mizigo; na

(b) pale inapowezekana, mistari ya ukomo wa upakiaji ya meli inakaguliwa mara kwa mara wakati wa kupakia au kupakua ili kuthibitisha takwimu za tani zinazotolewa.

(9) Uangalizi wa mistari ya ukomo wa upakiaji ya meli na tani uliorejewa chini ya kanuni ndogo ya (8) utarekodiwa kwenye kitabu cha kumbukumbu za mizigo na pale ambapo kuna utofauti mkubwa umegunduliwa kutoka kwenye mpango uliokubaliwa, mzigo au shughuli za farumi au vyote, utofauti huo utarekebishwa.

(10) Kwa madhumuni ya kanuni hii, mwakilishi wa kituo cha bandari maana yake ni mtu aliyeteuliwa na kituo cha bandari au kituo kingine, ambapo meli inapakia au kupakua, ambaye ana jukumu la kusimamia shughuli zinazofanywa na kituo cha bandari au kituo hicho kuhusiana na meli fulani.

## SEHEMU YA NNE
## UBEBAJI WA NAFAKA

Masharti ya meli ya mizigo inayobeba nafaka

**13**.-(1) Kwa kuzingatia masharti mengine yoyote yanayotumika chini ya Kanuni hizi, nahodha atahakikisha kwamba meli ya mizigo inayobeba nafaka-

(a) inazingatia masharti ya Kanuni za Kimataifa za Ubebaji wa Nafaka; na

(b) ina nyaraka za uidhinishaji kama inavyotakiwa chini ya Kanuni za Kimataifa za Ubebaji wa Nafaka.

(2) Shirika litahakikisha kwamba meli isiyo na nyaraka za udhinishaji haipakii nafaka hadi nahodha atakapoliridhisha Shirika kwamba meli inazingatia masharti ya Kanuni za Kimataifa za Ubebaji Nafaka katika hali yake ya upakiaji inayopendekezwa.

(3) Kwa madhumuni ya kanuni hii, masharti ya Kanuni za Kimataifa ya Ubebaji Nafaka yatakuwa ya lazima.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA JUMLA

Adhabu ya jumla

**14**. Mtu anayekiuka masharti yoyote ya Kanuni hizi, ambayo hakuna adhabu maalumu iliyotolewa, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi za Tanzania sawa na Dola za Marekani elfu moja au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita au vyote.

Tathmini na ripoti

**15**.-(1) Msajili-

(a) atafanya tathmini ya masharti ya udhibiti yaliyomo katika Kanuni hizi;

(b) ataandaa taarifa ya mchakato wa tathimini na kutoa hitimisho la mapitio; na

(c) atawasilisha taarifa kwa Waziri.

(2) Taarifa ya kwanza itawasilishwa kwa Waziri ndani ya miaka mitano kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Kanuni hizi.

(3) Taarifa zinazofuata zitawasilishwa kwa vipindi visivyozidi miaka mitano.

(4) Taarifa chini ya kanuni hii-

(a) itaweka malengo yanayokusudiwa kufikiwa na masharti ya udhibiti yanayorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1)(a);

(b) itatathmini kiwango ambacho malengo hayo yatafikiwa; na

(c) itatathmini endapo malengo hayo bado yanatija, na ikiwa ndivyo, itatathmini kiwango ambacho kinaweza kufikiwa kwa njia nyingine ya kiudhibiti ambayo si ngumu.

Ushughulikiaji wa malalamiko TS Na. 338 la 2018

**16**. Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi uliotolewa chini ya Kanuni hizi anaweza kuwasilisha malalamiko kwa Shirika kwa mujibu wa Kanuni za Ushughulikiaji wa Malalamiko za Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania za mwaka 2018.

---

**JEDWALI LA KWANZA**

---

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(2) (a))*

FOMU YA TAARIFA ZA MIZIGO

Zingatio: Fomu hii haitumiki ikiwa mzigo unaotakiwa kubebwa chini ya masharti ya sura ya VII, kanuni ya 5 ya Mkataba wa Usalama; Kiambatisho cha III, kanuni ya 4 ya MARPOL; na Utangulizi wa jumla wa kifungu cha 9 cha Kanuni za IMDG.

| | |
|---|---|
| Msafirishaji<br><br>…………………………………………………<br>……………… | Kumbukumbu namba<br><br>…………………………………………………<br>………………. |
| Mpokea mzigo | Mbebaji |
| Jina/njia ya usafirishaji.........................................................<br>...............<br><br>........................................................................... | Maelekezo ya masuala mengine<br>.........................................................................<br>...........................<br><br>......................................................................... |

| | |
|---|---|
| ..........................<br><br>Bandari/sehemu ya kuondoka...........................................................<br>..........................<br><br>..........................................................................<br>.......................... | .......................... |
| Bandari/sehemu ya kufikia<br><br>..........................................................................<br>.......................... | |
| Maelezo ya jumla ya mizigo<br><br>Aina ya bidhaa/ukubwa wa chembechembe<br><br>*Kwa shehena ya mizigo yabisi | Uzito wa jumla (kg/tani)<br><br>□ Mizigo ya jumla<br><br>□ Chombo cha kubebea mizigo.<br><br>□ Shehena ya mizigo |
| Maelezo ya shehena ya mizigo<br><br>Kigezo cha uhifadhi<br><br>Pembe iliyotengenezwa<br><br>Taratibu za kuweka sawa<br><br>Sifa za kemikali** ikiwa ni hatari<br><br>* kama inatumika<br><br>** Mfano daraja la IMO, Namba ya UN au Namba ya BC na Namba ya EmS. | |

| | |
|---|---|
| Sifa za kipekee za mizigo husika | Vyeti vya ziada*<br><br>Cheti cha kiwango cha unyevu na ukomo wa unyevu unaosafirishika<br><br>□ Cheti cha hali ya hewa |

| | |
|---|---|
| | □ Cheti cha msamaha<br>□ Nyingine (taja)<br>*kama inahitajika |
| TAMKO<br><br>Natamka hapa kwamba mizigo hiyo imeelezewa kikamilifu na kwa usahihi na kwamba matokeo yaliyotolewa ya vipimo na maelezo mengine ni sahihi kulingana na uelewa na ufahamu wangu na inaweza kuchukuliwa kuwa kuelezea mizigo itakayopakiwa. | |
| Jina na wadhifa.........................................................................................................................................................................<br><br>Kampuni/shirika la muwekaji saini.........................................................................................................................................<br><br>Mahali na tarehe .........................................................................................................................................................................<br><br>Saini kwa niaba ya msafirishaji………………………………………………………………………………………………… | |

*Fomu hii inakidhi masharti ya Sura ya VI na Kanuni ya 2 ya Mkataba wa Usalama, Kanuni za BC na Kanuni za CSS.*

**JEDWALI LA PILI**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni 8(8))*

MIONGOZO KWA AJILI YA MAANDALIZI YA MWONGOZO WA UFUNGAJI WA MIZIGO

UTANGULIZI

Kwa mujibu wa Sura za VI, VII za Mkataba wa Usalama na Kanuni za Taratibu za Uhifadhi na Utunzaji wa Mizigo (CSS Code), vyombo vya kubebea mizigo, ikijumuisha makasha, vitahifadhiwa na kutunzwa wakati wote wa safari kwa mujibu wa Mwongozo wa Uhifadhi wa Mizigo ulioidhinishwa na Shirika.

Mwongozo wa Ufungaji wa Mizigo unahitajika kwa aina zote za meli zinazojihusisha na ubebaji wa mizigo yote isipokuwa shehena za mizigo yabisi na oevu.

Madhumuni ya Miongozo hii ni kuhakikisha kwamba Miongozo ya Ufungaji wa Mizigo inazungumzia masuala yote ya uhifadhi na utunzaji mzigo na inatoa mbinu rasmi ya uandaaji wa Miongozo ya Kulinda Mizigo, mpangilio na maudhui yake. Shirika linaweza kuendelea kukubali Miongozo ya Uhifadhi wa Mizigo iliyoandaliwa kwa mujibu wa *Mwongozo wa Uhifadhi wa Mizigo -Makasha na Mizigo* ili mradi imekidhi masharti ya Miongozo hii.

Pale itakapobidi, Miongozo itapitiwa ipasavyo wakati meli inakusudiwa kubeba makasha katika mfumo sanifu.

Ni muhimu kwamba vifaa vya kufungia view vinakidhi vigezo vya utendaji na vya uthabiti vinavyokubalika na vinavyotumika katika meli na mzigo wake. Ni muhimu pia kwamba maafisa wa melini wawe na ufahamu wa ukubwa na uelekeo wa kani zinazohusika na kusahihisha matumizi na ukomo wa vifaa vya kufungia mizigo. Mabaharia na watu wengine walioajiriwa kwa ajili ya kufunga mizigo wanapaswa kuelekezwa juu ya matumizi sahihi ya vifaa vya kufungia mizigo melini.

**1 .1 Tafsiri**

"vifaa vya kufungia mizigo" maana yake ni vifaa visivyohamishika na vinavyohamishika vinavyotumika kufungia na kutegemeza vyombo vya kubebea mizigo;

"uwezo wa juu wa kufunga mzigo" maana yake ni uwezo unaokubalika wa mzigo kwa ajili ya kifaa kinachotumika kufungia mizigo kwenye meli. Uwezo wa kifaa kutenda kazi kwa usalama unaweza kubadilishwa kwa uwezo wa juu wa kufunga mzigo kwa madhumuni ya ufungaji, ilimradi hii itakuwa sawa na au itazidi uimara ulioelezewa na uwezo wa juu wa kufunga mzigo;

"mzigo uliosanifiwa" maana yake ni mzigo ambao meli imepewa mfumo ulioidhinishwa wa ufungaji kulingana na vyombo vya kubebea mizigo vya aina maalumu;

"mzigo uliosanifiwa nusu" maana yake ni mzigo ambao meli imepewa mfumo wa ufungaji wenye uwezo wa kuwa na ukomo wa aina ya vyombo vya kubebea mzigo, kama vile magari na trela; na

"mzigo usiosanifiwa" maana yake ni mzigo unaohitaji uhifadhi pekee na mipangilio ya ufungaji.

**1.2 Uandaaji wa mwongozo**

Mwongozo wa Ufungaji wa Mizigo utaandaliwa, kwa kuzingatia mapendekezo yaliyoainishwa kwenye Miongozo hii, na utaandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

**1.3 Taarifa za jumla**

Mwongozo utajumuisha taarifa za jumla zifuatazo:

(a) mwongozo uliotolewa humu hautaondoa kanuni bora za ubaharia, wala hautakuwa mbadala wa uzoefu katika utendaji wa uhifadhi na utendaji;

(b) taarifa na mahitaji yaliyowekwa katika Mwongozo yanashabihiana na mahitaji ya kitabu cha mlingano na ueleo thabiti wa meli, Cheti cha Kimataifa cha Mstari wa Kupakia, mwongozo wa uimara wa upakiaji wa umbo la meli pale itakapotolewa kwa mahitaji ya Kanuni za Kimataifa za Usafirishaji wa Bidhaa Hatarishi Majini pale inapohitajika;

(c) Mwongozo wa Kufunga Mizigo unaelezea mipangilio na vifaa vya kufungia mizigo vinavyopatikana ndani ya meli kwa matumizi sahihi kwa, na ufungaji wa vyombo vya kubebea mizigo, makasha, magari na vifaa vingine kwa kuzingatia kani mkingamo, mlalo na wima ambazo zinaweza kutokeza wakati wa hali mbaya ya hewa na mchafuko wa bahari.

(d) ni muhimu kwa ajili ya usalama wa meli na ulinzi wa mzigo na wafanyakazi, ufungaji wa mizigo ufanywe kwa usahihi na sehemu au viunga sahihi vya ufungaji vitumike kwa ajili ya ufungaji mzigo;

(e) vifaa vya kuhifadhia mizigo vilivyotajwa katika Mwongozo vitatumika kulingana na wingi, aina ya vifungashio na hali ya nje ya mzigo utakaobebwa;

(f) endapo aina mpya au mbadala wa vifaa vya kufungia mizigo vimetambulishwa, Mwongozo wa Ufungaji Mizigo utapitiwa upya ipasavyo na vifaa mbadala vya kufungia mizigo vilivyotambulishwa havipaswi kuwa na uimara mdogo kuliko vifaa vinavyobadilishwa;

(g) kutakuwa na kiasi cha kutosha cha vifaa vya akiba vya kufungia mizigo melini;

(h) taarifa kuhusu uimara na maelekezo ya matumizi na utunzaji ya kila aina mahususi ya kifaa cha kufungia mizigo, iwapo inahusika, itatolewa katika Mwongozo;

(i) kifaa cha kufungia mzigo kitatunzwa katika hali ya kuridhisha na vitu vilivyochoka au kuharibika katika kiwango ambacho ubora wake umeathiriwa, vitabadilishwa; na

(j) Mpango wa Ufikiaji Salama wa Mizigo utatoa taarifa za kina kwa watu wanaojihusisha na kazi zinazohusiana uhifadhi na ufungaji mizigo, na ufikiaji salama utatolewa na kudumishwa kwa mujibu wa Mpango huo.

**VIFAA VYA UFUNGAJI NA MIPANGILIO**

**2.1 Maelezo ya vifaa visivyohamishika vya kufungia mizigo**

Sehemu hii itabainisha na, endapo ni muhimu, kufafanua idadi, maeneo, aina na uwezo wa juu wa kufunga mzigo wa vifaa visivyohamishika vinavyotumika kufungia mizigo na kwa uchache kujumuisha taarifa zifuatazo:

(a) orodha au mpango wa vifaa visivyohamishika vya kufungia mizigo, ambavyo vitaambatishwa na nyaraka stahiki kwa kila aina ya kifaa kadiri iwezekanavyo, nyaraka zitajumuisha taarifa kuhusu-
- (i) jina la mzalishaji;
- (ii) aina ya matumizi ya kifaa mchoro rahisi kwa wepesi wa utambuzi;
- (iii) nyenzo;
- (iv) alama za utambuzi;
- (v) matokeo ya majaribio ya uimara au tamati ya mvutano;
- (vi) matokeo ya majaribio yasiyo uharibifu; na
- (vii) uwezo wa juu wa kufunga mzigo.

(b) vifaa vya ufungaji visivyohamishika kwenye kiambaza cha kukingama, fremu za webu, stanchi, na aina zake kama vile tundu, jicho la bolti, pale zinapotolewa, ikijumuisha uwezo wa juu wa kufunga mzigo;

(c) vifaa vya kufungia mizigo visivyohamishika kwenye deki na aina zake kama vile viunga vya miguu ya tembo, viunga vya kasha, vipenyo pale vinapotolewa, vikijumuisha uwezo wa juu wa kufunga mzigo;

(d) vifaa vya kufungia visivyohamishika kwenye sehemu za juu za deki, vinapotolewa, vikiorodhesha aina zake na uwezo wa juu wa kufunga mzigo; na

(e) kwa meli zilizopo ambazo hazina vifaa visivyohamishika ambavyo vimesanifiwa, taarifa kuhusu uwezo wa juu wa kufunga mzigo na sehemu za kufungia zinaonekana toshelezi.

**2.2 Maelezo ya vifaa vinavyohamishika vya kufungia mizigo**

Sehemu hii itabainisha idadi ya sifa za utendaji na za muundo wa vifaa vinavyohamishika vya kufungia mizigo vinavyobebwa melini, vitaambatishwa na michoro au vielelezo stahiki, vinavyojumuisha taarifa zifuatazo:

(a) orodha ya vifaa vinavyohamishika vya kufungia mizigo, ambavyo vitaambatishwa na nyaraka sahihi kwa kila aina ya kifaa, ambazo zitajumuisha taarifa kuhusu:
- (i) jina la mzalishaji;
- (ii) aina ya matumizi ya kifaa mchoro rahisi kwa wepesi wa utambuzi;
- (iii) nyenzo, ikijumuisha kiwango cha chini cha halijoto ya uendeshaji salama;
- (iv) alama za utambuzi;
- (v) matokeo ya majaribio ya uimara au tamati ya mvutano;
- (vi) matokeo ya majaribio yasiyo uharibifu; na
- (vii) uwezo wa juu wa kufunga mzigo.

(b) Viunga vya kuunganisha fito za makasha, viunga vya kufungia kasha kwenye deki, viunga vya kufungia makasha yaliyobebana, kiunganishi cha safu mbili za makasha, uwezo wa juu wa kufunga mzigo na matumizi;

(c) minyororo, waya wa kufungia, ufito, uwezo wa juu wa kufunga mizigo na matumizi;

(d) mikazo kama vile viungashi fito, mikazo ya mnyororo, uwezo wa juu wa kufunga mzigo na matumizi;
(e) zana za kufungia magari, na vyombo vya moto vingine, uwezo wa juu wa kufunga mzigo na matumizi;
(f) egemeo na jeki, kwa ajili ya vyombo vya moto ikijumuisha matrela endapo yametolewa, uwezo wa juu wa kufunga mzigo na matumizi; na
(g) nyenzo za kuzuia kuteleza kama vile mbao laini za kutumiwa na vyombo kubebea mizigo zenye sifa za kiwango kidogo za msuguano.

**2.3 Mipango ya ukaguzi na matengenezo**

Sehemu hii itaelezea mipango ya ukaguzi na matengenezo ya vifaa vya kufungia mizigo melini.

2.3.1 Ukaguzi na matengenezo ya mara kwa mara yatafanyika chini ya uangalizi wa nahodha na ukaguzi wa vifaa vya kufungia mizigo kwa uchache zitajumuisha-

(a) uchunguzi wa mara kwa mara wa vifaa vinavyotumika; na
(b) uchunguzi wa mara kwa mara au kupimwa upya kama itakavyohitajika na Shirika na vifaa husika vya kufungia mizigo vitafanyiwa ukaguzi endapo utahitajika.

2.3.2 Sehemu hii itabainisha namna ya kutunza kumbukumbu za hatua za ukaguzi na matengenezo ya vifaa vya kufungia mizigo melini na taarifa zitaingizwa katika kitabu cha kumbukumbu za mafuta, kitakachowekwa na Mwongozo wa kufunga Mizigo.Kitabu cha kumbukumbu kitajumuisha taarifa zifuatazo:

(a) taratibu za kukubali, kutengeneza na kukarabati au kukataa vifaa vya kufungia mizigo; na
(b) kumbukumbu za ukaguzi.

2.3.3 Sehemu hii itajumuisha taarifa kwa ajili ya nahodha kuhusu ukaguzi na marekebisho ya mipangilio ya ufungaji wakati wa safari.

2.3.4 Taratibu za matengenezo zilizowekwa kielektroniki zinaweza kurejewa katika Sehemu hii.

**UHIFADHI NA UFUNGAJI WA MIZIGO ISIYO SANIFIWA NA ILIYOSANIFIWA NUSU**

**3.1 Maelekezo ya usalama na ubebaji**

Sehemu hii itakuwa na taarifa zifuatazo:

(a) maelekezo kuhusu ubebaji wa vifaa vya kufungia; na
(b) maelekezo ya usalama kuhusiana na ubebaji wa vifaa na vyombo vya kufungia na kufungulia kwenye meli na kwa watu waliopo nchi kavu.

**3.2 Tathmini ya kani zinazozalishwa kwenye vyombo vya kubebea mzigo**

Sehemu hii itakuwa na taarifa zifuatazo:

(a) majedwali au michoro inayotoa muhtasari mpana wa kani za mseleleko zinazotarajiwa kutokea sehemu mbalimbali za meli wakati wa hali ya mchafuko wa bahari katika wigo wa kimo cha metasentriki kinachoweza kutumika;
(b) mifano ya kani zinazozalishwa kwenye vyombo vya kubebea mzigo vinapokabiliwa na kani za mseleleko ziliorejewa katika aya (a) na thamani za pembe za myumbo wa meli na kimo cha metasentriki ambapo kani zinazozalishwa kwenye vyombo vya kubebea mzigo zinazidi kikomo kinachoruhusiwa kwa mipangilio ya ufungaji maalumu;
(c) mifano ya jinsi ya kukokotoa idadi na uimara wa vifaa vya kufungia vinavyohamishika vinavyohitajika kukabiliana na kani zinazorejewa katika aya

(b) na vile vile vigezo vya kiusalama vitakavyotumika kwa aina tofauti za vifaa vya kufungia mizigo vinavyohamishika, mahesabu yanaweza kufanywa kulingana na Kiambatisho cha 13 cha Kanuni za CSS au mbinu zilizokubaliwa na Shirika;

(d) inapendekezwa kuwa mbunifu wa Mwongozo wa Kufungia Mizigo abadilishe njia ya kukokotoa iliyotumika kwenye fomu kulingana na meli husika, vifaa vyake vya kufungia na mizigo iliyobebwa na fomu hiyo inaweza kuwa na michoro inayotumika, majedwali au mifano iliyokokotolewa; na

(e) mipangilio mingine ya uendeshaji kama vile kuchakata data kielektroniki au matumizi ya kompyuta ya kupakia vinaweza kukubaliwa kama masharti ya aya (a) hadi (d), iwapo kwamba mfumo una taarifa sawa.

**3.3 Matumizi ya vifaa vya kufungia vinavyohamishika kwenye vyombo vya kubebea mizigo mbalimbali, vyombo vya moto na vizuizi vya kuhifadhia mizigo**

3.3.1Sehemu hii itazingatia nahodha kwenye matumizi sahihi ya vifaa vya kufungia mzigo vinavyohamishika, kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo, kama vilivyoonyeshwa kwenye Kiambatisho cha 13 cha Kanuni za CSS-

(a) muda wa safari;

(b) eneo la kijiografia la safari kwa kuzingatia kiwango cha chini cha hali joto la vifaa vya kufungia mzigo vinavyohamishika;

(c) hali ya bahari inayoweza kutarajiwa;

(d) vipimo, muundo na sifa za meli;

(e) kani tuli na kani mwendo zinazotarajiwa wakati wa safari;

(f) aina na ufungaji wa vyombo vya kubebea mzigo na vyombo vya moto;

(g) mtindo unaokusudiwa wa uhifadhi wa vyombo vya kubebea mzigo na vyombo vya moto; na

(h) maada na vipimo vya vyombo vya kubebea na vyombo vya moto.

3.3.2 Sehemu hii itaelezea matumizi ya vifaa vya kufungia mizigo vinavyohamishika kama idadi ya mifungo na pembe za mifungo zilizoruhusiwa, ambapo ni muhimu, maandishi yataongezwa kwa michoro au vielelezo vinavyofaa ili kuwezesha uelewa sahihi na matumizi sahihi ya vifaa vya kufungia aina mbalimbali za mzigo na vifaa vya kubebea mizigo.

3.3.3 Kwa vyombo vya kubebea mizigo fulani na vitu vyenye ukinzani wa msuguano mdogo,inashauriwa kuweka mbao laini au nyenzo nyingine za kuzuia utelezi chini ya mizigo ili kuongeza msuguano kati ya deki na mizigo.

3.3.4 Sehemu hii itakuwa na mwongozo wa mahali na njia inayopendekezwa ya kuhifadhi na kufunga kasha, trela na vyombo vya moto vingine vya kubeba mizigo, mizigo inayobebwa kwenye toroli, vyombo vya mizigo na mzigo mmoja kama vile mbao, miviringisho ya karatasi, mizigo, magari na vyombo vya moto vingine.

3.3.5 Wakati mifungo inayotegemea hali ya hewa, taratibu za uendeshaji zitatengenezwa kwa mujibu wa Kiambatisho cha 13 cha Kanuni cha CSS.

**3.4 Masharti ya ziada kwa meli za ro-ro**

3.4.1 Mwongozo utakuwa na vielelezo vinavyoonyesha mpangilio wa vifaa vya kufungia mzigo visivyohamishika vikiwa na utambulisho wa uimara, uwezo wa juu wa kufunga mzigo pamoja na umbali wa mkingamo na wima kati ya sehemu za kufungia, katika kuandaa sehemu hii mwongozo zaidi utatumika kutoka kwenye maazimio ya Shirika la Bahari

Duniani juu ya vipengele vitakavyoweza kuzingatiwa wakati wa Kuzingatia uhifadhi salama na ufungaji wa vyombo vya kubebea Mizigo na vyombo vya moto kwenye meli na miongozo kwa mipangilio ya ufungaji kwa usafirshaji wa vyombo vya moto barabarani na meli za ro-ro.

3.4.2 Katika kubuni mipangilio ya ufungaji kwa vyombo vya kubebea mizigo, kujumuisha vyombo vya moto na makasha, kwenye meli za ro-ro na abiria na kubainisha mahitaji ya chini ya uimara kwa vifaa vya kufungia mizigo vilivyotumika, kani kutokana na mjongeo wa meli, pembe ya myumbo baada ya uharibifu au mafuriko na mazingatio mengine kuhusiana na ufanisi wa mipangilio ya ufungaji wa mzigo.

**3.5 Meli za kubeba shehena**

Pale ambapo meli za kubeba shehena zimebeba vyombo vya kubebea mzigo vilivyomo kwenye mawanda ya sura ya VI/5 au sura ya VII/5 ya Mkataba wa Usalama, mzigo huo utahifadhiwa na kufungwa mujibu wa Mwongozo wa Kufunga Mizigo.

**UHIFADHI NA UFUNGAJI WA MAKASHA NA MIZIGO MINGINE ILIYOSANIFIWA**

**4.1 Maelekezo ya utunzaji na usalama**

Sehemu hii itakuwa na:

(a) maelekezo kuhusu utunzaji sahihi wa vifaa vya ufungaji; na

(b) maelekezo ya usalama yanayohusiana na utunzaji wa vifaa vya ufungaji na makasha yaliyofungwa na yasiyofungwa au mizigo mingine iliyosanifiwa na mfanyakazi aliye melini au asiye melini.

**4.2 Maelekezo ya uhifadhi na ufungaji**

Sehemu hii inatumika kwa mfumo wowote wa uhifadhi na ufungaji kama vile uhifadhi ndani au bila ya kutumia chumba cha kuhufadhia makasha na mizigo mingine iliyosanifiwa. Kwenye meli zilizopo nyaraka zinazohusika na uhifadhi na ufungaji salama zinaweza kuunganishwa kwenye nyenzo zinazotumiwa kwa uandaaji kama ilivyoainishwa chini ya aya ya 4.2 hadi 4.4.

4.2.1 Mpango wa uhifadhi na ufungaji

Sehemu hii itakuwa na mpango wa kina na unaoeleweka au seti za mipango inayotoa muhtasari muhimu kuhusu:

(a) muonekano wa urefu na wa pande zote wa mahali pa kufungia makasha chini na juu ya deki;

(b) mifumo mbadala ya uhifadhi makasha yenye vipimo tofauti;

(c) uzito wa juu wa kasha unaoweza kubebwa juu ya kasha jingine;

(d) mfuatano wa kubebanisha makasha wima unaokubalika;

(e) ukomo wa urefu wa kubebanisha makasha kuhusiana na njia za kuona zilizoidhinishwa; na

(f) utumiaji wa vifaa vya kufungia kwa kutumia alama zinazofaa kwa kuzingatia nafasi ya kuhifadhi, uzito wa kasha, mfuatano wa kubebanisha makasha, urefu wa kubebanisha makasha, alama zitakazotumika zitakuwa sawa katika Mwongozo wa Ufungaji wa Mizigo.

4.2.2 Kanuni ya uhifadhi na ufungaji kwenye deki na chini ya deki.

4.2.2.1 Sehemu hii itasaidia tafsiri ya Mpango wa Uhifadhi na Ufungaji kuhusu uhifadhi wa makasha ikielezea:

(a) umatumizi ya vifaa vilivyoainishwa; na

(b) Mwongozo wowote au ukomo wa vipimo kama vile ukubwa wa makasha, uzito wa juu wa kasha unaoweza kubebwa juu ya kasha jingine, mfuatano wa

kubebesha makasha, ubebanishaji wa makasha ulioathiriwa na upepo, urefu wa makasha yaliyobebanishwa.

4.2.2.2 Itajumuisha tahadhari mahususi za madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi mabaya ya vifaa vya kufungia mizigo au tafsiri potofu ya maelekezo yaliyotolewa.

**4.3 Mifumo mingine inayoruhusiwa ya uhifadhi**

4.3.1 Sehemu hii itatoa taarifa muhimu kwa nahodha kushughulikia hali za uhifadhi wa mizigo kinyume na maelekezo ya jumla yaliyoelezewa chini ya sehemu ya 4.2, ikijumuisha tahadhari zinazofaa za madhara yanayoweza kutokea, maonyo yanayofaa ya matokeo yanayoweza kutokea kutokana na matumizi mabaya ya vifaa vya kufungia mizigo au tafsiri potofu ya maelekezo yaliyotolewa.

4.3.2 Pamoja na mambo mengine, taarifa itatolewa kuhusu:

(a) mpangilio mbadala wa kubebanisha makasha wima;
(b) ubebanishaji wa makasha ulioathiriwa na upepo kwa kukosekana kwa makasha ya nje yaliyobebabishwa;
(c) uhifadhi mbadala wa makasha yenye vipimo mbalimbali; na
(d) upunguzaji unaoruhusiwa wa juhudi za ufungaji kuhusiana na uzito wa makasha ya safu za chini, urefu wa makasha mepesi yaliyobebanishwa au sababu nyingine.

**4.4 Nguvu inayotumika kwenye vyombo vya kubebea mizigo**

4.4.1 Sehemu hii inahusu usambazaji wa kuongeza kasi ambayo mfumo wa uhifadhi na ufungaji mizigo unategemea, na kutaja hali ya msingi ya utulivu.

4.4.2 Taarifa juu ya nguvu zinazochochewa na upepo na bahari kwenye mzigo wa uliopo kwenye deki.

4.4.3 Taarifa kuhusu ongezeko la kawaida la nguvu au uharakishaji na ongezeko la uthabiti wa awali na mapendekezo yatatolewa kwa ajili ya kupunguza hatari ya upotevu wa mizigo kutoka kwenye deki kwa uzito au urefu wa makasha yaliyobebanishwa, ambapo uthabiti wa juu wa awali hauwezi kuepukika.

**MPANGO WA KUPATIKANA KWA MIZIGO**

5.1 Meli ambazo zimeundwa mahususi na kuwekwa kwa madhumuni ya kubeba makontena zitapewa Mpango wa Ufikiaji Salama wa Mizigo (CSAP) ili kuonyesha kwamba wafanyakazi watakuwa na ufikiaji salama kwa shughuli za ulinzi wa kontena.

5.2 Mpango huo utaeleza kwa kina mipangilio muhimu ya kuhifadhi mizigo kwa njia salama na kujumuisha yafuatayo kwa maeneo yote yatakayofanyiwa kazi na wafanyakazi:

(a) mikondo;
(b) majukwaa;
(c) njia za kutembelea;
(d) ngazi;
(e) ufikiaji wa vifuniko;
(f) eneo la vifaa vya kuhifadhia;
(g) vifaa vya taa;
(h) upangaji wa kontena kwenye vifuniko vya kuanguliwa au nguzo;
(i) vifaa vya kuweka vyombo maalumu, kama vile plagi za rifa au vyombo;
(j) vituo vya huduma ya kwanza na ufikiaji au njia ya dharura;

*Tangazo la Serikali Na. 381 (Linaendelea)*

(k) magenge; na

(l) mipango mingine yoyote muhimu kwa utoaji wa njia ya usalama.

5.3 Miongozo ya mahitaji mahususi itakuwa kama inavyotolewa katika kiambatisho 14 cha Kanuni za CSS

Dodoma,
3 Mei, 2024

MAKAME M. MBARAWA
*Waziri wa Uchukuzi*